

Taarifa ya Chanjo ya COVID-19

Watu wa mji wetu sasa hivi wanapata chajo ya COVID-19.

Hizi ni taarifa za muhimu kuhusu Chanjo ya COVID-19



Chanjo ni bure kwa kila mtu. Unaweza kuulizwa utoe taarifa za bima kipindi unajiandikisha. Ila bima haihitajiki kwaajili ya kupata chanjo.

Chanjo haitibu COVID-19, nausaidia mwili wako kujikinga na COVID-19.

Hauwezi kupata maambukizi ya COVID-19 kutoka kwenye chanjo.

Kama tayari umepata COVID-19 bado unapaswa kupata chanjo.

Chanjo haisimamiwi na serikali au muunganiko wa serikari.

Usambazaji

Usambazaji unasimamiwa kupitia idara za afya za serikali. Kwa taarifa zaidi tembelea:

- healthvermont.gov
- health.ny.gov

Makampuni ya Chanjo

Kuanzia Machi 1 kuna chanjo tatu zinazopatikana kutokana na Idhini ya Dharura: Pfizer, Moderna na Johnson & Johnson. Wote Pfizer na Moderna wanahitaji risasi mbili.

- Pfizer: siku 21 kati ya dozi, Moderna: siku 28 kati ya dozi
- Dozi zote mbili unazopokea zitakuwa kutoka kwa mtengenezaji mmoja wa chanjo.

Chanjo za ziada zinaweza kupatikana.

Ufanisi

Ili Chanjo iwe na ufanisi, inahitajika upate dozi zote.

Ufanisi wa chanjo dhidi ya milipuko mipya bado unachunguzwa, na matokeo yake yanaleta faraja. Hii bado inaangaliwa kwa ukaribu zaidi na kutafitiwa.

Athari

Athari ndogo kutokana na chanjo ni kawaida na haimaanishi kuwa una COVID. Dalili zinaweza kuwa:

- Dalili kama za mafua masaa 24-36
- Uchovu
- Maumivu ya mikono
- Maumivu ya kichwa

Athari hizi zina uwezekano mkubwa kutokea baada ya dozi ya pili.



Mzio

Kuwa na mzio hakukufanyi usiwe na vigezo vya kupata chanjo.

Kama umewahi kuwa na mzio mkali sababu ya chanjo au dawa (inayokuhitaji kupata msaada wa haraka wa kiafya) hapo mwanzo, ni muhimu kujadili na daktari wako kabla ya kupata chanjo.

Kustahiki

Watu wenye upungufu wa kinga bado wanaweza kupata chanjo. Hii inajumuisha watu wenye HIV, magonjwa ya moyo, astma, matatizo ya utumbo, na sickle cell.

Umri: Chanjo ya Moderna imethibitishwa kwa umri wa miaka 18+ na Pfizer imethibitishwa kwa umri wa miaka 16+

Ujauzito & unyonyeshaji: Chanjo inawafaa watu ambao ni wajaazito au wanao nyonyesha. Watu wenye ujauzito wanaweza kupata chanjo pale kundi la 'hali ya hatari linapostahili.

Kinga

Taadhari lazima zinahitajika bado ziwepo hadi pale watu wakutosha wawe wamepata chanjo, ambapo itakuwa miezi mingi kutoka sasa.

Unahitajika:

- Kuvaa barakoa
- Kunawa mikono
- Kuwa mbali futi 6 kutoka kwa mtu moja hadi mwengine wakati upo inje ya nyumbani kwako.
- Kutokuwa na mikusanyiko

Taarifa za kiimani

Chanjo ni Kosher.

Chanjo ni Halali.

Hakuna vinasaba vya binadamu wala mnyama kwenye chanjo.

Kama una maswali yoyote ya ziada au wasiwasi kuhusu Chanjo ya COVID-19, tunakusihia uwasiliane na daktari wako.

Kama utahitaji msaada juu ya uandikishwaji wa chanjo juu ya kizuizi cha lugha, tafadhali wasiliana na AALV, USCRI au VT LEND.

Taarifa hii imetengenezwa kwa ushirikiano na AALV, USCRI Vermont, na VT LEND.

**Kwa taarifa zaidi tembelea:
UVMHealth.org/Coronavirus**